

AJILI YA MIZIGO AFRICA CARGO

Sisi ni nani?

Mizigo africa cargo ni kampuni ya kimataifa mjini Brussels, maalumu katika usafirisaji wa mizigo kwa hewa na bahari.

Je huduma zetu ni zipi?

Sisi tunakusanya mizigo kutoka kwa nyumba za wateja wetu na tunasafirisha kwa ghala letu ambapo zoezi la kufunga na kupima uzito wa mizigo unafanyika. Baada ya hapo tunasafirisha ile mizigo kwa hewa ama kwa bahari. Wafanyikazi wetu waliopo ile nchi mizigo inatumwa, wataipokea na wasafirishe hiyo mizigo kwa anwani ya mwenye hio mizigo.

Aidha, sisi hutoa huduma ya mlango kwa mlango kati ya Ulaya , Afrika na nyinginezo nchi ulimwenguni. Huduma hii kati ya africa na ulaya, utoaji dhamana ya mizigo ndani ya upeo wa masaa 48.

Mfano; mteja wetu anatupatia mizigo kwa ajili ya kuisafirisha Kigali, Kinshasa ama Bujumbura jumatatu saa 10.00 asubuhi, sisi tuna upeleka kwa ghala letu na kuufunga ule mizigo, kisha tunaupima ili tujue uzito wake. Tukisha maliza tunauchukua na kuupeleka kwa kiwanja cha ndege cha brussels. Ule mizigo utasafirishwa siku inayofuatia jumanne saa 10.00 asubuhi ndio uweze kufika africa siku hiyo hiyo saa 19.00 jioni. Wafanyikazi wetu waliopo kwa hiyo nchi wataupokea kisha wasafirishe kwa anwani ya myenye hou mizigo jumatano kabla ya saa 10.00 asubuhi.

Ufungaji wetu unafanya kwa jinsi gani?

Kutegemea na mizigo inayosafirishwa, sisi tunahakikisha ufungaji bora ili kuzuia mizigo kutokana na uharibifu wowote.

Kama vile, carton, masanduku ya mbao, pallets za plastiki, pallets za mbao, karatasi za plastiki zilizo na hewa ndani kwa ajili ya mizigo kama vile Fridges, Tv, Hi-Fi, vyombo vya jikoni nakadhalika.

Mizigo Africa cargo twaenda kwa kasi !

Kwanini uchague Mizigo Africa cargo?

Sisi ni kampuni ya kipekee inayotoa huduma ya mlango kwa mlango kwa mikoa mbalimbali kwa bei ya kipekee na hakuna gharama za ziada zozote. Viwango ushindani huenda mkono kwa mkono na huduma zetu bora kwa wateja wetu wote.

Kuhakikisha kuridhika kwa wateja wetu ni kipaumbele chetu kikuu!

Vile vile bidhaa na fedha ni vipini vinavyo angaliwa kwa uangalifu na busara ya kipekee.

Mizigo Africa cargo twaenda kwa kasi !

Timu yetu

Katika usafirisaji wa mizigo kwa hewa, wafanyikazi wetu ni maalufu kwa ustadi wao katika usafirisaji na vifaa visafi.

Sisi tunao ujuzi kwa mawasiliano bora kwa wateja wetu kwa lugha mbalimbali kama vile Kifaransa, Kiingereza, Kiswahili, Kinyarwanda na Kidutch.

Timu yetu ina uwezo na ujuzi na uchambuzi kuhakikisha mahusiano bora kwa wateja wetu.

Kwanini Mizigo Africa ni zaidi ya kampuni zingine za meli?

Mbali na huduma zetu washirika wetu ni wamiliki wa meli na ni maalum kwa usafirishaji wa magari na vyombo katika bahari.

Usafiri wetu wa mtandao unajumuisha bandari kuu kati ya ulaya na mabara mengine.

Sisi huchukua huduma za taratibu zote za forodha kwa niaba ya wateja wetu.

Huduma ya ukusanyaji na ufungaji wa mizigo ni bure.

Kuridhika kwa mteja wetu ni kipaumbele chetu kikuu!

Mizigo Africa cargo twaenda kwa kasi!

Kwenda maili ya ziada

Huduma mpya kwa wateja wetu waaminifu

Ununuzi wa bidhaa kwa niaba yao.

Kama kwa sababu yoyote mteja wetu hawezi kusafiri kwa marudio yoyote iwe Africa, Ulaya ama ingineyo nchi, mizigo cargo inachukua hilo jitihada la kutafuta, kununua na kutuma ile bidhaa mteja wetu anahitaji kwa upeo wa masaa 48 kima cha chini kwa upeo wa siku saba.

Vilevile mteja wetu atatakiwa kulipa ada ya usindikaji. Kumbuka kwamba 50% ya hiyo ada itarudishwa.

Ada ya usindikaji na ada ya bidhaa lazima ilipwe kwa fedha za ndani katika nchi husika na katika akaunti ambayo maelezo yake yatapatianwa.

Jinsi unaweza wasiliana

28 Rue Frans Pepermans
1140 Evere – Belgium

simu ya mkononi +32 (0)4 85 750 560

Simu +32(0)2 374 63 00

Emai;. info@mizigocargo.com

Website; www.mizigocargo.com